Jarida la DCEA TOLEO LA KWANZA JANUARI - JUNI, 2022 ISSN NO. 978 - 9912 - 9896 - 1 - 0

# DAWA ZA KULEVYA

Kataa Dawa za Kulevya, Timiza Malengo Yako

## Ifahamu

### Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya



HALIUZWI

Kamishna Jenerali Gerald Musabila Kusaya

Kishindo cha Kusaya Uk.2

Serikali kushirikiana na sekta binafsi kudhibiti uchepushaji wa kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya Uk.11

Mafanikio ya Miaka 60 ya Uhuru katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya Uk.13



# Yaliyomo


Kishindo cha Kusaya >>> Uk.2



Madhara ya matumizi na biashara ya dawa za kulevya Uk.3

Uraibu wa dawa za kulevya Uk.5

Matukio Pichani >>>



Uk.6-9

Serikali kushirikiana na sekta binafsi kudhibiti uchepushaji wa kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya Uk.11



Ifahamu Sheria ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya >>> Uk.12

Mafanikio ya Miaka 60 ya Uhuru katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya Uk.13

Katuni Uk.17-18

# Ni jukumu letu sote kupambana na tatizo la dawa za kulevya

*NCHI yetu inakabiliwa na tatizo la dawa za kulevya hasa bangi na mirungi ambazo huzalishwa hapa Nchini zikifuatiwa na dawa aina nyingine zinazoingizwa kutoka nje kama heroin na cocaine. Aidha, kumekuwepo na matumizi ya dawa tiba zenye asili ya kulevya ambazo pia zinachangia kuathiri nguvu kazi ya taifa.*

*Katika kudhibiti tatizo la dawa za kulevya Mamlaka hutekeleza majukumu yake kwa kufuata mihimili mikuu minne ambayo ni; kudhibiti upatikanaji, kupunguza uhitaji, kupunguza madhara yanayotokana na matumizi ya dawa za kulevya pamoja na kukuza ushirikiano wa kikanda na kimataifa katika kupambana na tatizo hilo.*

*Katika kudhibiti upatikanaji wa dawa za kulevya, Mamlaka hufanya operesheni mbalimbali za ukamataji na uteketezaji wa dawa hizo. Aidha, imeendelea kutoa elimu kwa jamii juu ya madhara yanayotokana na matumizi na biashara ya dawa za kulevya ili jamii isijiingize kwenye matumizi ya dawa hizo. Mamlaka imekuwa ikiratibu na kusimamia matibabu kwa waraibu wa dawa za kulevya ili kupunguza madhara yanayotokana na matumizi ya dawa hizo. Pia, Mapambano dhidi ya tatizo la dawa za kulevya yanahitaji ushirikiano wa kikanda na Kimataifa. Katika kutekeleza hilo, nchi yetu inashiriki katika kutekeleza makubaliano ya mpango kazi wa miaka mitano (2019 -2023) wa Sera ya Kimataifa ya kuimarisha mapambano ya dawa za kulevya katika ngazi ya nchi, kanda na Kimataifa ili kuweka nguvu ya pamoja katika kutatua tatizo la dawa za kulevya Duniani.*

*Ni wajibu wa kila mwananchi kutoa taarifa juu ya watu wanaojihusisha na biashara ya dawa za kulevya, lengo likiwa kuifanya nchi yetu kuwa huru na kuwa na kizazi kisichotumia wala kushiriki biashara ya dawa za kulevya.*



*Gerald Musabila Kusaya*
***Kamishna Jenerali***

*Picha ya Jarida*



*Gerald Musabila Kusaya*
*Kamishna Jenerali DCEA*

**Jarida hili limeandaliwa na**
Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya

**WAHARIRI**

*Gerald Musabila Kusaya*
***Mhariri Mkuu***

*Florence Khambi*
***Mhariri***

*Daniel Kasokola*
***Mhariri Msaidizi***

*Lilian Matho*
***Mhariri Msaidizi***

**SHUKURANI**

*Issa Muhidin Michuzi*

*Faustine Kapama*

*Said Mwinshehe*

*Mussa Ngarango Jr.*

*Haji Abeid*

**MAWASILIANO:**

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya
S.L.P 80327
Dar es Salaam

8 Barabara ya Kivukoni,
11486 Dar es Salaam

**Simu:** +255 22 211 3754/57
**Nukushi:** +255 22 211 3752
**Barua pepe:** cg@dcea.go.tz
info@dcea.go.tz

@dceatanzania
@dceatanzania
@dcea tanzania
DCEATV
www.dcea.go.tz

***Namba ya Mawasiliano Bila Malipo (Call Centre) 119***

# Ifahamu Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) ni Taasisi ya Serikali iliyoko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Mamlaka hii ilianzishwa kwa Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Na. 5 ya Mwaka 2015 na kuanza kufanya kazi rasmi mwezi Februari, 2017.

## Majukumu ya Mamlaka:

Majukumu ya Mamlaka kama yalivyoainishwa chini ya kifungu cha 4 cha Sheria Namba 5 ya mwaka 2015, ni kufafanua, kuhamasisha udhibiti wa dawa za kulevya, kuratibu na kutekeleza hatua zote zinazoelekezwa katika udhibiti wa dawa za kulevya.

Katika kutekeleza majukumu hayo Mamlaka inafanya kazi zifuatazo:

- **i.** Kusimamia utekelezaji wa mikataba ya kimataifa, maazimio na makubaliano katika kudhibiti dawa za kulevya;
- **ii.** Kuandaa na kutekeleza mpango wa Taifa wa kudhibiti dawa za kulevya;
- **iii.** Kutengeneza miongozo inayoelezea tatizo la dawa za kulevya na madhara yake katika jamii;
- **iv.** Kuboresha na kurekebisha sheria na kanuni za udhibiti wa dawa za kulevya;
- **v.** Kuhamasisha udhibiti wa matumizi na biashara ya dawa za kulevya ikiwemo kutoa elimu juu ya madhara ya dawa za kulevya, kusambaza taarifa kwa umma na juhudi nyingine za udhibiti;
- **vi.** Kuchukua hatua stahiki za kupambana na biashara ya dawa za kulevya zikiwemo kukamata, kupekua na kufanya uchunguzi wa masuala yanayohusiana na dawa za kulevya;
- **vii.** Kuzuia, kupeleleza na kuchunguza uchepushwaji wa dawa za tiba zenye madhara ya kulevya pamoja na kemikali zilizosajiliwa kutoka kwenye vyanzo halali wakati huo huo kuhakikisha dawa hizo zinapatikana kwa matumizi ya tiba, biashara na mahitaji ya kisayansi;
- **viii.** Kuanzisha mfumo thabiti wa ukusanyaji taarifa na uchambuzi katika ngazi ya Taifa kuhusu matumizi na biashara ya dawa za kulevya;
- **ix.** Kuhamasisha, kuratibu na kuhakikisha jitihada za ushirikiano wa kimataifa katika kudhibiti wa dawa za kulevya zinaimarishwa;
- **x.** Kufanya, kuwezesha na kuratibu tafiti zinazohusiana na dawa za kulevya;
- **xi.** Kuratibu na kuwezesha wadau wanaojihusisha na udhibiti wa matumizi na biashara ya dawa za kulevya;
- **xii.** Kuelimisha na kuhamasisha jamii kushiriki katika mapambano dhidi ya matumizi na biashara ya dawa za kulevya;
- **xiii.** Kutoa mafunzo kwa watendaji wanaojihusisha na udhibiti wa matumizi na biashara ya dawa za kulevya, fedha haramu na kemikali bashirifu;
- **xiv.** Kufanya uchunguzi wa sayansi jinai.

## Misingi Muhimu:

### Uadilifu

Kuzingatia kanuni za uadilifu na ukweli ili kutenda haki bila upendeleo.

### Ushirikiano

Kuimarisha ushirikiano na wadau pamoja na jumuiya ya kimataifa katika jitihada za kupambana na kudhibiti dawa za kulevya.

### Uwajibikaji

Kufanya kazi kwa kuzingatia maslahi ya umma ili kuilinda jamii dhidi ya matumizi, biashara na madhara ya dawa za kulevya.

### Ubunifu

Matumizi ya njia/mbinu bora zaidi zinazokidhi kutatua changamoto mpya katika udhibiti wa dawa za kulevya.

### Weledi

Kuwa na timu ya wataalamu wanaofanya kazi kwa weledi na maarifa.

### Usiri

Kuweka siri ya vyanzo vya taarifa za dawa za kulevya ili kuwalinda watoa taarifa.

### Ufanisi

Kufanya kazi kwa bidii na maarifa ili kutimiza malengo.

Katika kutekeleza majukumu hayo, Mamlaka inashirikiana na Taasisi nyingine za Kitaifa na Kimataifa, Asasi za kiraia, Vyombo vya habari na jamii kwa ujumla.

# Kishindo cha Kusaya

*Ukamataji mkubwa kufanyika kwa mara moja tangu kuanzishwa kwa Mamlaka hii.*



*KILO 859.36 za dawa za kulevya zilizokamatwa ndani ya jahazi eneo la Kilwa Masoko Mkoani Lindi zikiwahusisha raia saba wa Iran.*

**Na FLORENCE Khambi**

TAREHE 4 Aprili, 2021, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan alimteua Gerald Musabila Kusaya kuwa Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Nchini. Wiki mbili baadaye, Mamlaka ilifanikiwa kukamata jumla ya kilo 859.36 za dawa za kulevya zikijumuisha kilo 504.36 za heroin na kilo 355 za methamphetamine. Huu ni ukamataji mkubwa kuwahi kufanyika kwa mara moja katika historia ya mapambano dhidi ya dawa za kulevya Nchini. Miezi miwili baadaye, Mamlaka ilifanikiwa kukamata kilo 88.27 za dawa za kulevya zikijumuisha kilo 76.02 za methamphetamine na kilo 12.25 za heroin.

Katika kipindi cha mwezi Aprili hadi Oktoba 2021, jumla ya hekari 11 za bangi ziliteketezwa mkoani Pwani, kilo 89.01 za bangi zilikamatwa katika maeneo tofauti, jumla ya hekari 10 za shamba la mirungi ziliteketezwa na bunda 170 za mirungi zilikamatwa wilayani Same, Kilimanjaro.

Ukamataji huu umepunguza usambazaji wa dawa za kulevya Nchini na kusababisha uhaba wa dawa hizo na kuwafanya waraibu kutafuta tiba katika vituo mbalimbali vya kutolea huduma.

Aidha, katika kipindi hicho vituo sita vya kutolea huduma ya tiba ya methadone vimefunguliwa Nchini. Kati ya hivyo, vituo vidogo vinne (Satellite clinics) vilifunguliwa katika jiji la Dar es Salaam na vituo vikubwa viwili vilifunguliwa mikoa ya Arusha (Mount Meru) na Songwe (Tunduma). Vituo vingine vinapatikana katika mikoa ya Dar es Salaam, Mbeya, Mwanza, Dodoma, Tanga, na Pwani. Mpaka sasa kuna jumla ya vituo 15 Nchini. Vituo hivi kwa pamoja vimeweza kusajili na kuhudumia waraibu wapatao 10,600.

Katika kutekeleza majukumu yake, Kamishna Jenerali Kusaya amekuwa akisema ni jukumu lake kuwatumikia watanzania katika kusimamia mapambano dhidi ya tatizo la dawa za kulevya na hatimaye kuifikia Tanzania huru isiyokuwa na kizazi kinachotumia wala kushiriki katika biashara ya dawa za kulevya.

Mafanikio haya yamewezekana kutokana na utashi wa kisiasa katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya, ambapo Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, amekuwa mstari wa mbele kuviwezesha vyombo vinavyojihusisha na udhibiti wa dawa hizo Nchini.

# Madhara ya matumizi na biashara ya dawa za kulevya

*...Pia husababisha kukithiri kwa vitendo vya kihalifu*

**Na LILIAN Matho**

DAWA za kulevya ni kemikali ambazo zikiingia mwilini huathiri mfumo wa fahamu hasa ubongo wa mtumiaji na kuleta mabadiliko ya kihisia, kifikra na kitabia tofauti na matarajio ya jamii. Dawa hizi hutokana na mimea na kemikali ambazo ni malighafi muhimu kwa mahitaji mengine ya mwanadamu. Dawa hizi huingia mwilini kwa njia kuu ya kunywa/kula, kuvuta na kujidunga sindano.

Kuna namna nyingi ya kuzigawa dawa za kulevya. Kwa muktadha huu dawa za kulevya zimegawanywa kwa vigezo vya madhara yanayosababishwa na dawa husika kwenye mfumo wa fahamu na kutokana na namna zinavyozalishwa.

## Kundi la dawa za kulevya kulingana na madhara kwenye mfumo wa fahamu:

Kuna makundi makuu matatu ya dawa za kulevya kulingana na athari zake kwenye mfumo huo. Makundi hayo ni vichangamshi, vipumbaza na vileta njozi. Vichangamshi huongeza kasi ya utendaji wa mfumo wa fahamu hivyo kuongeza mapigo ya moyo na kasi ya kupumua. mfano cocaine, mirungi na dawa jamii ya amphetamine; vipumbaza (depressants) hupunguza kasi ya utendaji wa mfumo wa fahamu hivyo kushusha mapigo ya moyo, kasi ya kupumua na utendaji wa akili mfano heroin na valium; vileta njozi (Hallucinogens) huleta hisia na maono yasiyokuwepo kutokana na kuvurugwa kwa utendaji wa milango ya fahamu. Mtumiaji huona, husikia, huhisi, hunusa na hata kupata ladha tofauti na uhalisia, mfano bangi.

## Kundi la dawa za kulevya kulingana na uzalishaji:

Kundi hili limegawanyika katika sehemu tatu: dawa za kulevya halisia zinazotokana na mimea kama bangi na mirungi, dawa za kulevya zinazopatikana kutokana na kuchanganywa kwa kemikali na mimea halisia kama heroin na cocaine pamoja na dawa za kulevya zinazotengenezwa viwandani kwa kutumia kemikali bashirifu pekee kama methamphetamine.



*JAMII na Serikali huingia gharama zisizo za lazima kwa ajili ya ukamataji, matibabu ya waraibu.*

Matumizi na biashara ya dawa za kulevya yana madhara kiafya, kijamii, kiuchumi, kisiasa na kimazingira.

**Kiafya;** Matumizi ya dawa za kulevya husababisha magonjwa mbalimbali yakiwemo afya ya akili, uraibu, moyo, homa ya ini, kifua kikuu na vifo vya ghafla. Aidha, huchangia kuenea kwa maambukizi ya VVU hasa miongoni mwa watumiaji wa dawa hizo kwa njia ya kujidunga. Matumizi hayo yanaweza kufanya mishipa ya

*Inaendelea Ukurasa wa 4*

# Madhara ya dawa za kulevya

*Inatoka Ukurasa wa 3*

damu kusinyaa na inapotokea hali hiyo kwenye ubongo husababisha shinikizo la damu na kiharusi, hupunguza uwezo wa kufikiri na kufanya maamuzi sahihi. Dawa za kulevya pia husababisha saratani, hupunguza nguvu za kiume, kuoza meno na vidonda kwenye mfumo wa chakula. Wanawake wajawazito wanaweza kujifungua watoto wenye uraibu wa dawa za kulevya na waliodumaa kimwili na kiakili.

**Kijamii;** dawa za kulevya husababisha kukithiri kwa vitendo vya kihalifu katika jamii kama wizi, ukahaba, utapeli na uporaji na kuifanya jamii kuishi kwa woga. Huvuruga mahusiano katika familia na kusababisha talaka, uwepo wa watoto wa mitaani na utoro shuleni. Aidha, watumiaji wa dawa za kulevya wamekuwa wakinyanyapaliwa katika jamii hali inayosababisha wakose haki zao za kifamilia na kijamii na hata pale wanapoacha matumizi ya dawa za kulevya familia zao au waajiri hushindwa kuwakubali.

**Kiuchumi;** dawa za kulevya hudhoofisha afya za watumiaji na kuwafanya washindwe kushiriki katika shughuli za uzalishaji. Biashara ya dawa za kulevya husababisha mfumuko wa bei na kuondoa mizania ya ushindani wa kibiashara kwa kuwa wafanyabiashara wa dawa za kulevya wana uwezo wa kununua bidhaa kwa bei ya juu kuliko bei ya kawaida ya soko hivyo kuwakosesha wengine fursa na kuongeza pengo la kipato kati yao na wananchi wa kawaida hali inayosababisha kushuka kwa thamani ya fedha na kuzorotesha ukuaji wa uchumi.

Jamii na Serikali huingia gharama zisizo za lazima kwa ajili ya matibabu ya waraibu, kutoa elimu ya kupunguza matumizi ya dawa za kulevya, ukamataji wa wafanyabiashara wa dawa za kulevya, kutunza wafungwa gerezani, badala ya kuelekeza rasilimali hizo kwenye maendeleo hivyo kurudisha nyuma jitihada za kukuza uchumi wa nchi.

**Kisiasa;** Kutokana na uwezo mkubwa wa kifedha wa wafanyabiashara wa dawa za kulevya wanaweza kujipenyeza katika shughuli za kisiasa kwa kufadhili chaguzi au kuwaondoa viongozi waliochaguliwa kidemokrasia na kuwaweka watu wao madarakani ili kulinda maslahi yao. Hivyo kuwepo na uwezekano wa nchi kupata viongozi wasio waadilifu.

**Kimazingira;** Kilimo cha bangi na mirungi hufanyika kwenye milima na misitu kwa kutaka miti na kuharibu uoto wa asili hivyo kusababisha kukauka kwa vyanzo vya maji, ukame, mmomonyoko wa ardhi na kutoweka kwa baadhi ya viumbe hai na uoto wa asili. Uharibifu huu umejidhihirisha katika baadhi ya safu za milima ya Uluguru, Usambara, Udzungwa, Upare na maeneo ya Arumeru.

Kutokana na madhara haya, Mamlaka kwa kushirikiana na wadau wengine hutoa elimu juu ya madhara ya dawa za kulevya katika makundi mbalimbali ya kijamii ili kujenga ufahamu juu ya tatizo hilo. Elimu hiyo inalenga kuiepusha jamii isijiingize kwenye matumizi na biashara ya dawa za kulevya na kupunguza madhara yatokanayo na dawa za kulevya kwenye jamii na kwa watumiaji.



*KAMISHNA Msaidizi wa Kinga na masuala ya Kijamii Bi. Moza Makumbuli akitoa elimu juu ya tatizo la dawa za kulevya kwa waandishi wa habari za kidijitali.*

# Uraibu wa dawa za kulevya

## *Jamii itambue kuwa uraibu ni ugonjwa na unatibika*

**Na LILIAN Matho**

URAIBU wa dawa za kulevya ni ugonjwa sugu unaotokana na matumizi ya dawa za kulevya ambao huathiri ubongo hasa upande wa fikra, hisia na tabia. Hali hii humfanya mtumiaji kuwa na uhitaji wa lazima wa dawa za kulevya huku akijua madhara yanayotokana na matumizi ya dawa hizo .

Mtumiaji anapotumia dawa za kulevya kwa njia yoyote ile, dawa hizo huingia kwenye damu kisha kwenda kwenye sehemu ya ubongo ambayo kitaalamu huitwa *limbic system*. Sehemu hii inahusika na kuleta msisimko kwa mtumiaji. Dawa za kulevya zikifika kwenye ubongo, husababisha kutolewa kwa wingi kwa kemikali iitwayo Dopamine. Kemikali hii ndiyo inayo husika na kuleta raha, hivyo kumfanya mtumiaji kuendelea kutumia dawa za kulevya. Mtumiaji hulazimika kuongeza kiasi cha dawa anayoitumia ili kufikia raha anayoihitaji na mwisho huwa tegemezi wa dawa hizo.

## Matibabu kwa waraibu wa dawa za kulevya:

Kuna aina mbalimbali za matibabu kwa waraibu wa dawa za kulevya ingawa hakuna tiba moja ambayo inafaa kwa waraibu wote. Matibabu ya uraibu wa dawa za kulevya hutofautiana sana kulingana na aina ya dawa husika, kiasi cha dawa kilichotumika, muda wa uraibu, matatizo ya kiafya na mahitaji ya kijamii na mtu binafsi.

**Huduma za tiba ya uraibu zinazotolewa Nchini ni;** Tiba saidizi kwa waraibu kwa kutumia dawa (Medically Assisted Therapy - MAT), Huduma katika Nyumba za Upataji Nafuu (Sober Houses) na Tiba kwenye vituo vya kutolea Huduma za Afya ya Akili. Hata hivyo, kuna baadhi ya waraibu wanaopatiwa huduma za unasihi pekee kwenye asasi za kiraia na kuachana na matumizi ya dawa hizo.

**Huduma ya tiba saidizi kwa waraibu kwa kutumia dawa (MAT);** huambatana na ushauri nasaha kwa waraibu wanaotumia dawa za kulevya aina ya afyuni kama vile heroin na baadhi ya dawa tiba zenye asili ya kulevya. Pia huhusisha tiba kwa magonjwa yaambatanayo na matumizi ya dawa za kulevya kama vile magonjwa ya akili, UKIMWI, kifua kikuu, magonjwa ya ngono na homa ya ini. Utaratibu wa utoaji huduma huanza kwa asasi za kiraia kuwaibua na kuwaandaa waraibu katika ngazi ya jamii ambapo waraibu hupata elimu na huduma ya unasihi kabla ya kufikishwa katika vituo vya tiba saidizi.

Huduma ya MAT Nchini ilianza mwaka 2011 katika kliniki moja iliyopo ndani ya Hospitali ya Taifa Muhimbili. Hadi kufikia mwezi Desemba, mwaka 2021 jumla ya kliniki 15 zilikuwa zinatoa huduma hiyo Tanzania bara. Kliniki za methadone zipo kwenye hospitali ya Taifa Muhimbili na hospitali za rufaa za Mwananyamala na Temeke - Dar es Salaam, Hospitali ya Tumbi - Pwani, Meta - Mbeya, Sekou Toure – Mwanza , Bombo - Tanga, Mount Meru - Arusha. Vituo vingine vinavyotoa huduma hiyo ni Itega jijini Dodoma, hospitali ya wilaya ya Bagamoyo na zahanati ya Tunduma Songwe.

Aidha, Serikali imeendelea kupanua huduma hiyo kwa kuongeza vituo vingine vidogo vinne (satelite clinics) jijini Dar es Salaam katika zahanati za Mbagala Round Table, hospitali ya Vijibweni Kigamboni, zahanati ya Tegeta Kinondoni na kituo cha afya cha gereza la Segerea. Pia ina mpango wa kuanzisha vituo vingine sehemu mbalimbali Nchini. Waraibu wa dawa wa aina zote wanatakiwa kuhudhuria matibabu kila siku kwa angalau miaka mitatu.

**Huduma katika nyumba za upataji nafuu;** huendeshwa na asasi za kiraia ambapo waraibu wa dawa za kulevya wanapata huduma kwa kupitishwa kwenye hatua 12 za upataji nafuu bila kutumia dawa ya aina yoyote. Matibabu haya hutolewa kwa malipo kwa waraibu wa dawa zote za kulevya kwa muda usiopungua miezi minne. Serikali inaratibu uanzishwaji na kusimamia uendeshwaji wa Nyumba za Upataji Nafuu kwa kutumia Mwongozo wa Uanzishaji na Uendeshaji wa Nyumba za Upataji Nafuu Tanzania Bara. Hadi kufikia mwezi Desemba 2021; kulikuwa na jumla ya nyumba 43 zinazotoa huduma hiyo katika mikoa ya Kilimanjaro, Tanga, Dar es Salaam, Pwani, Dodoma, Morogoro, Iringa, Mwanza, Kagera, Tabora na Arusha.

Katika huduma hii watumiaji wa dawa za kulevya husaidiana wenyewe kwa wenyewe ambapo waraibu waliopata nafuu (kuacha matumizi ya dawa hizo kwa

*Inaendelea Ukurasa wa 6*



KAMISHNA Jenerali wa Mamlaka (wa pili kushoto) na wajumbe wengine wakiwa kwenye mkutano wa 64 wa Kamisheni ya Kimataifa ya Kudhibiti Dawa za Kulevya jijini Vienna - Austria.

# Tanzania yashirikiana kimataifa Kudhibiti dawa za kulevya

**Na DANIEL Kasokola**

UJUMBE kutoka Tanzania ukiongozwa na Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) ulishiriki katika Mkutano wa 64 wa Kamisheni ya Umoja wa Mataifa ya Kudhibiti wa Dawa za Kulevya (CND) uliofanyika mwezi Oktoba , 2021 jijini Vienna – Austria.

Mkutano huo huwa na lengo la kubadilishana uzoefu, kuimarisha ushirikiano wa kikanda na Kimataifa pamoja na kutatua changamoto zinazojitokeza katika mapambano dhidi ya tatizo la dawa za kulevya.



KAMISHNA Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), Gerald Musabila Kusaya (kulia),akibadilishana mawazo na baadhi ya viongozi wa UNODC wakati wa mkutano huo.

Pamoja na masuala mengine, mkutano huo ulijadili namna bora ya kupambana na tatizo la dawa za kulevya na makosa mengine ya uhalifu wa kupangwa ikiwemo ugaidi, utakatishaji fedha, usafirishaji haramu wa binadamu, uhalifu wa kimtandao, kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa pamoja na namna bora ya kutatua changamoto zinazojitokeza katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya Duniani.

# Uraibu wa dawa za kulevya

*Inatoka Ukurasa wa 5*

kipindi kisichopungua mwaka mmoja) huwaongoza waraibu wanaojiunga kushiriki mikutano ya ustiri wa mihadarati (Narcotic Anonymous) ambapo hupitishwa kwenye hatua kumi na mbili za upataji nafuu pamoja na unasihi. Waraibu wanaojiunga huweza hupatiwa mafunzo ya ujasiriamali, kazi za mikono pamoja na kushiriki katika shughuli za michezo.

**Tiba kwenye vituo vya kutolea Huduma za Afya ya Akili;** Huduma hizi hutolewa katika zahanati, vituo vya afya na kwenye vitengo vya afya ya akili na dawa za kulevya katika hospitali za rufaa. Mara nyingi watumiaji wa dawa za kulevya huwa na magonjwa mbalimbali ya afya ya akili hivyo vituo hivi hutoa suluhisho kwa tatizo la afya ya akili na utegemezi wa dawa za kulevya.

**Huduma ya unasihi;** Huduma hii hutolewa kwenye asasi zinazowahudumia waraibu wa dawa za kulevya, nyumba za upataji nafuu, vituo vya kutolea huduma za afya ya akili na dawa za kulevya pamoja na vituo vya MAT. Watumiaji wengi wa dawa za kulevya huwa na sababu mbalimbali zinazowafanya kujiingiza kwenye matumizi ya dawa hizo ambazo huweza kupatiwa ufumbuzi kupitia huduma hii.

Jamii inapaswa kutambua kuwa, uraibu ni ugonjwa unaotibika. Hivyo, ina wajibu wa kutowanyanyapaa waraibu na badala yake iwaelekeze na kuwasaidia kupata tiba.

# *Katika kujenga mahusiano, Mamlaka inafanya kazi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya.*



*KAMISHNA Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Gerald Musabila Kusaya alipotembelea ofisi za Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC), zilizopo barabara ya Pugu na Mikocheni jijini Dar es Salaam. Lengo la ziara hii ni kujifunza, kuimarisha mahusiano mazuri yaliyokuwepo kati ya Mamlaka na shirika hilo ili kuweka mikakati madhubuti katika kuuhabarisha Umma juu ya tatizo la dawa za kulevya.*





*VIONGOZI wa Mamlaka walipotembelea ofisi ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), kuona namna shughuli za uchunguzi wa kimaabara wa sampuli za dawa za kulevya unavyofanyika.*



*KAMISHNA Jenerali Kusaya na viongozi wengine walipotembelea ofisi ya Baraza la Famasia, Dodoma kwa lengo la kuimarisha mifumo ya kupeana taarifa za uchepushwaji wa dawa tiba zenye asili ya kulevya na kuendelea kushirikiana kufanya tafiti za pamoja na kuweka mikakati katika udhibiti wa dawa za kulevya.*




*WAZIRI Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa (katikati), aliyekuwa Waziri wa Nchi ofisi ya Waziri Mkuu, kazi, vijana, ajira na watu wenye ulemavu Mhe. Jenista Mhagama, Mwenyekiti wa Mkutano wa 28 wa wakuu wa vyombo vya udhibiti wa dawa za kulevya nchi za Afrika (HONLEA ) na aliyekuwa Kamishna Jenerali wa Mamlaka Rogers Siyanga (kulia) na ujumbe kutoka UNODC wakati wa ufunguzi wa mkutano wa HONLEA uliofanyika Nchini Tanzania.*

*Picha na Daniel Kasokola*



*KILO 268.50 za dawa za kulevya aina ya heroin zilizokamatwa eneo la Mbezi Kibanda cha Mkaa jijini Dar es Salaam.*



*MAAFISA wa Mamlaka wakifafanua jambo juu ya tatizo la dawa za kulevya kwa baadhi ya wananchi waliotembelea banda la Mamlaka katika kilele cha siku ya kimataifa ya kupambana na dawa za kulevya.*



*KAMISHNA Jenerali akimuonesha sampuli ya dawa za kulevya mgeni rasmi aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mhe. George Simbachawene (Mb) kwenye kilele cha maadhimisho ya Siku ya Kupambana na Dawa za Kulevya Duniani tarehe 26 Juni, 2021.*



*MAKAMU wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Othman Masoud, aliyekuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar Dkt. Saada Mkuya, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge inayoshughulika na masuala ya UKIMWI, Dawa za Kulevya na Magonjwa yasiyoambukizwa Fatma Toufiq, Kamishna Jenerali, pamoja na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar, Kanali Burhan Zubeir Nassor wakiwa katika picha ya pamoja.*




*Maafisa wa DCEA na wadau mbalimbali wakiwa kwenye zoezi la uteketezaji wa dawa za kulevya.*



*KITUO cha MAT katika hospitali ya mount Meru jijini Arusha.*



*DAMIAN Jankowisyki Kryzstof raia wa Poland akifikishwa Mahakama ya Hakimu Mkazi Moshi kusomewa hukumu yake ambapo alihukumiwa kifungo cha miaka 30 jela baada ya kukutwa na kosa la kulima miche 729 ya bangi na kusafirisha kilo 17.2 za aina hiyo ya dawa za kulevya .*

# Mashauri ya dawa za kulevya

**Na LILIAN Matho**

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ina jukumu la kuhakikisha kuwa ukamataji wa wafanyabiashara wa dawa za kulevya unafata taratibu za ukamataji kama zilivyoainishwa chini ya kifungu cha 48 cha Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya. Aidha, kifungu hiki kinasaidia katika kuharakisha ukamilishaji wa upelelezi na kuhakikisha watuhumiwa wanafikishwa mahakamani kwa wakati.

Mamlaka kwa kushirikiana na wadau wa Haki Jinai ikiwemo Mahakama kupitia vikao vya kusukuma mashauri, wamekuwa wakijadili na kuweka malengo mbalimbali ya kuhakikisha mashauri ya Jinai yakiwemo ya Dawa za Kulevya yanamalizika kwa wakati.

Tangu kuanzishwa kwa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya mwezi Februari 2017 hadi Desemba 2021, jumla ya mashauri 6,894 ya kesi zinazohusu dawa za kulevya yamefunguliwa katika Mahakama mbalimbali Nchini. Katika Mashauri hayo jumla ya kesi 336 zimetolewa maamuzi na kati ya hizo Jamhuri imeshinda kesi 243. Mashauri mengine bado yanaendelea mahakamani katika hatua mbalimbali.

**152.63**

*Baadhi ya mashauri yaliyomalizika Mahakamani kwa mafanikio ni Shauri la Uhujumu Uchumi 1/2020 lilihusisha gramu 152.63 za heroin katika Mahakama Kuu Kanda ya Tanga.*

Baadhi ya mashauri yaliyomalizika Mahakamani kwa mafanikio ni Shauri la Uhujumu Uchumi Namba 1/2020 lilihusisha gramu 152.63 za heroin katika Mahakama Kuu Kanda ya Tanga. Katika Shauri hili mtuhumiwa alitiwa hatiani na kufungwa miaka 30 jela.

Pia, kesi Namba 5/2015 iliyohusisha dawa za kulevya aina ya heroin gramu 275.40 katika Mahakama Kuu kitengo cha Uhujumu Uchumi ambapo watuhumiwa walitiwa hatiani na kufungwa kifungo cha maisha. Vilevile shauri la Jinai namba 79/2020 lililohusisha kilimo na usafirishaji wa bangi katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Moshi, watuhumiwa walikutwa na hatia na kuhukumiwa kutumikia kifungo cha miaka 30 jela.

# Serikali kushirikiana na sekta binafsi kudhibiti uchepushaji wa kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya



*Kamishna Jenerali wa DCEA, Gerald Musabila Kusaya akisaini makubaliano ya kushirikiana na Sekta binafsi katika mapambano dhidi ya kemikali bashirifu na dawa za tiba zenye asili ya kulevya huku akishuhudiwa na Mkemia Mkuu wa Serikali Dkt. Fidelice Mafumiko.*

**Na LILIAN Matho**

SERIKALI kupitia Mamlaka imeingia makubaliano na kampuni zinazojihusisha na uingizaji, usafirishaji, usambazaji na utumiaji wa kemikali bashirifu pamoja na vyama vinavyojihusisha na dawa tiba zenye asili ya kulevya kwa lengo la kuimarisha udhibiti wa uchepushwaji wa kemikali bashirifu ili zisitumike kutengeneza dawa za kulevya na dawa tiba zenye asili ya kulevya zisitumike kama dawa za kulevya.

**31/8/2021**

*Tarehe iliyofanyika utiaji saini Dar es Salaam*

Makubaliano hayo yamefanyika kwa kutia saini hati ya makubaliano (MoU) kati ya Serikali na sekta binafsi ambazo ni kampuni 32 zinazojihusisha na kemikali bashirifu na vyama viwili ambavyo ni Tanzania Pharmaceutical Manufacturers Association (TPMA) na Tanzania Association of Pharmaceutical Industries (TAPI) vinavyowakilisha zaidi ya wanachama 134 ili kushiriki katika kuzuia uchepushwaji wa bidhaa hizo.

Utiaji saini huo ulifanyika tarehe 31 Agosti, 2021 jijini Dar es Salaam, kati ya wakurugenzi wa kampuni na wenyeviti wa vyama hivyo (TAPI na TPMA) na Kamishna Jenerali wa Mamlaka ambaye aliziwakilisha Taasisi za Serikali za Udhibiti wa Kemikali na Dawa za Binadamu. Tukio hilo lilishuhudiwa na Mkemia Mkuu wa Serikali Dkt. Fidelice Mafumiko pamoja na wawakilishi kutoka Taasisi za Serikali za Udhibiti ambazo ni Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), Bohari Kuu ya Dawa (MSD), Baraza la Famasia (PC), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na Mamlaka ya Bandari (TPA).

Kati ya Mwaka 2015 na mwaka 2017 Tanzania ilikuwa kwenye changamoto ya usafirishaji haramu wa kemikali bashirifu na kufanywa kama kituo cha kusafirishia bidhaa hizo. Kemikali bashirifu ni kemikali za kawaida zenye matumizi halali ila zikichepushwa huweza kutumika katika mchakato wa kutengeneza dawa za kulevya.

Serikali imeendelea kuimarisha udhibiti wa kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya kwa kuweka utaratibu wa matumizi salama wa bidhaa hizo kupitia Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Viwandani na Majumbani Namba 3 ya mwaka 2003, Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Namba 5 ya mwaka 2015 na Sheria ya Dawa na Vifaa Tiba ya mwaka 2019.

Ushirikiano huu utaimarisha nguvu ya udhibiti wa kemikali bashirifu pamoja na dawa tiba zenye asili ya kulevya ili kuliepusha taifa letu na tatizo la dawa za kulevya.

# Ifahamu Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya



*MAOFISA kutoka Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya na maofisa wa ofisi ya Mwendesha Mashtaka Nchini waliposhiriki kikao kazi kilicholenga kubadilishana uzoefu juu ya uendeshaji wa mashauri ya dawa za kulevya Nchini.*

**Na DANIEL Kasokola**

MAPAMBANO dhidi ya dawa za kulevya Nchini yanaongozwa na Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za kulevya. Sheria hiyo inaharamisha mambo mbalimbali yakiwemo; kilimo cha bangi, mirungi, kumiliki mbegu zinazozalisha dawa za kulevya, inaharamisha usafirishaji wa dawa za kulevya, kujihusisha kwa namna yoyote kinyume cha sheria na kemikali bashirifu, kumiliki mashine, vifaa na maabara kwa lengo la kutengeneza dawa za kulevya.

**1995**

*Mwaka ambao ilianzishwa iliyokuwa Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya iliyokuwa na jukumu la kuhamasisha, kuainisha na kuratibu utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Kudhibiti dawa za kulevya*

Sheria inaipa Mamlaka uwezo wa kukamata, kupekua na kupeleleza kesi. Aidha, Sheria hiyo inaipa uwezo Serikali kuanzisha na kusimamia vituo vya tiba kwa waraibu (kifungu cha 31), inaipa uwezo Mamlaka kuratibu shughuli zinazofanywa na wadau za kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya, kutoa elimu juu ya tatizo la dawa za kulevya, kuziwezesha asasi za kiraia zinazotoa elimu juu tatizo la dawa za kulevya, kuandaa miongozo mbalimbali inayohusu dawa za kulevya pamoja na madhara yake kwa jamii (kifungu cha 4).

Sheria Chini ya kifungu cha 63 inatambua uanzishaji wa huduma za tiba au huduma za kupunguza athari kwa waraibu. Aidha, kifungu cha 31 kinaruhusu tiba kwa waraibu wa dawa za kulevya. Kifungu hicho kinaipa uwezo Mahakama kuruhusu mraibu wa dawa za kulevya baada ya kutiwa hatiani kwa hiari yake kupata tiba.

Katika Sheria hiyo, makosa ya dawa za kulevya za viwandani mfano heroin na cocaine kuanzia gramu 20 na kuendelea hayana dhamana. Aidha, kwa makosa ya dawa za kulevya zinazozalishwa hapa nchini mfano bangi na mirungi kuanzia kilo 20 na kuendelea hayana dhamana. Pia, mtuhumiwa akitiwa hatiani kwa kosa la kujihusisha na biashara ya dawa za kulevya za viwandani mfano heroin na cocaine zenye uzito wa kuanzia gramu 200 na kuendelea ni kifungo cha maisha. Sheria inatoa kifungo cha miaka 30 kwa kujihusisha na kilimo cha dawa za kulevya mfano bangi na mirungi.

Kosa la kumiliki, kusafirisha, kemikali bashirifu zenye uzito zaidi ya lita 100 ikiwa kwenye hali ya kimiminika na kilo 100 ikiwa kwenye hali ya yabisi adhabu yake ni kifungo cha maisha. Sheria haitoi dhamana kwa mtuhumiwa atakayetiwa hatiani kwa makosa ya kemikali tajwa endapo kemikali hizo zitakuwa na uzito wa kilo 30 au lita 30 na kuendelea.

Serikali kupitia Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya imeazimia kupambana vilivyo na wafanyabiashara wa dawa za kulevya na kuhakikisha tatizo la dawa hizi linakuwa historia Nchini. Hivyo, itaendelea kuboresha Sheria na Kanuni zake ili kuongeza tija na ufanisi katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya.

# Mafanikio ya Miaka 60 ya Uhuru katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya

## *Watuhumiwa 45,784 wamekamatwa kutoka mwaka 2017 hadi 2021*

**Na FLORENCE Khambi**

MAMLAKA imetekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020 - 2025 Ibara ya 245 (a-e) ambayo inaelekeza utekelezaji wa masuala mbalimbali katika kudhibiti dawa za kulevya Nchini kama yalivyoainishwa kwenye Ibara hiyo.

Serikali ilitunga Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Namba 5 ya Mwaka 2015 pamoja na kuanzisha Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya. Sheria hii imeendelea kuboreshwa kwa kufanyiwa marekebisho mara kwa mara mara ili kuendana na wakati kwa kuwa mbinu za usafirishaji wa dawa za kulevya hubadilika mara kwa mara.

Katika kubaini na Kuvunja Mitandao mikubwa ya Dawa za Kulevya Nchini, Mamlaka kwa kushirikiana na Taasisi mbalimbali za Kimataifa kama vile UNODC, Interpol, DEA, CIA na NCA imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kudhoofisha na kuvunja mitandao mikubwa ya wafanyabiashara wa dawa za kulevya ndani na nje ya nchi. Wengi wao wamekamatwa na mashauri yao yapo mahakamani, baadhi yao wanatumikia vifungo hadi vya maisha na wengine wamekimbia nje ya nchi. Kwa mujibu wa taarifa ya mwaka 2019 ya Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Masuala ya Dawa za Kulevya na Uhalifu (UNODC), nchi ya Tanzania ilifanikiwa kupunguza uingizaji wa dawa za kulevya moja kwa moja kutoka kwa nchi zalishaji kwa zaidi ya asilimia 90.

> **15**
>
> *Mamlaka kwa kushirikiana na iliyokuwa Wizara ya Afya pamoja na Asasi za Kiraia imefikisha vituo 15 mwaka 2021 kutoka kituo kimoja mwaka 2011*

Tangu kuanzishwa kwa Mamlaka mwaka 2017 hadi kufikia 2021, operesheni mbalimbali za ukamataji wa wafanyabiashara wa dawa za kulevya zimefanyika na kufanikisha kukamatwa kwa jumla ya watuhumiwa 45,784. Kati yao 2,231 wa heroin, 502 cocaine, 37,743 bangi na 5,308 wa mirungi.

Aidha, dawa za kulevya zilizokamatwa ni kilo 1125.41 za heroin, kilo 26.67 za cocaine, tani 199.74 za bangi, tani 97.64 za mirungi, tani 57.6 za Kemikali Bashirifu, Kilo 431.02 za Methamphetamine, na Mashamba ya bangi 49 yenye jumla ya ekari 56.

Aidha, ukamataji uliofanyika tarehe 24 Aprili, 2021 wa kilo 859.36 za dawa za kulevya ukihusisha watuhumiwa saba raia wa Iran waliokamatwa katika Bahari ya Hindi eneo la Kilwa Masoko mkoani Lindi umevunja rekodi na kuwa ukamataji wa kwanza wa kilo nyingi zilizokamatwa kwa pamoja toka Nchi yetu ipate uhuru.

Mamlaka kwa kushirikiana na Wizara ya Afya pamoja na Asasi za Kiraia imefanikiwa kupanua huduma za tiba kwa waraibu wa dawa za kulevya nchini, kutoka kituo kimoja mwaka 2011 hadi kufikia vituo 15 mwaka 2021. Mwaka 2016 kulikuwa na vituo vitatu vikiwahudumia waraibu 3,500 kwa siku. Aidha, hadi kufikia mwaka 2021 idadi ya waraibu iliongezeka na kufika 10,600 ambao hupata huduma kwa siku katika jumla ya vituo 15. Serikali imeendelea kusimamia uanzishaji na uendeshaji wa Nyumba za Upataji Nafuu ambapo kuanzia mwaka 2012 hadi mwaka 2021 jumla ya nyumba 43 zilisajiliwa.

Kutoa elimu kuhusu madhara ya Dawa za Kulevya pamoja na udhibiti wa uchepushwaji wa kemikali bashirifu kupitia vilabu vya kupinga dawa za kulevya shuleni, vyombo vya habari, warsha za kitaifa na makongamano. Hii imesaidia kwa kiasi kikubwa kuzuia wimbi la vijana kuingia kwenye matumizi na biashara ya dawa hizo. Aidha, Mamlaka imezijengea uwezo Asasi za kiraia 70 ambazo zinatoa elimu juu ya madhara ya dawa za kulevya katika jamii katika mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Pwani, Tanga, Arusha, Mbeya, Songwe na Mtwara.

Katika kutekeleza sheria ya Kudhibiti na Kupambana na dawa za kulevya, Mamlaka ilifanikiwa kufungua jumla ya kesi 6,894 katika Mahakama mbalimbali Nchini. Jumla ya kesi 336 zilitolewa maamuzi mahakamani na kati ya hizo Jamhuri ilishinda kesi 243.

# Mamlaka yang'ara tuzo za uandaaji wa taarifa za fedha viwango vya kimataifa



**Na DANIEL Kasokola**

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) imekuwa mshindi wa kwanza na kupata tuzo mbili za umahiri katika uandaaji wa taarifa za fedha ya mwaka 2020 kwa viwango vya kimataifa kwa sekta za Umma (IPSA) katika kundi la Wizara na Idara za Serikali zinazojitegemea (MDAs).

Tuzo ya kwanza ni tuzo ya umahiri katika uandaaji wa taarifa za fedha ya mwaka 2020 kwa viwango vya kimataifa kwa sekta za umma (IPSA) katika kundi la Wizara naTaasisi za Serikali zinazojitegemea (MDAs) na tuzo ya pili ni ya mshindi wa jumla kwa Wizara, Mashirika na Mabenki.

Mamlaka imekuwa mshindi wa kwanza na kupata tuzo hii mara nne mfululizo tangu mwaka 2018. Ushindi huu umechagizwa na usimamizi mzuri wa masuala ya fedha ndani ya Mamlaka na kupata hati safi kila mwaka ambayo ni kigezo pekee za kuingia kwenye washindano hayo.




Mbali na kazi ya kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya, Kamishna Jenerali Gerald

## 2020

*Tuzo ya kwanza ni tuzo ya umahiri katika uandaaji wa taarifa za fedha ya mwaka 2020 kwa viwango vya kimataifa kwa sekta za umma (IPSA) katika kundi la Wizara naTaasisi za Serikali zinazojitegemea (MDAs)*

Kusaya huweka jitihada katika kuangalia jinsi ambavyo rasilimali fedha zinatumika kama ilivyokusudiwa ikiwa ni pamoja na kuweka vizuri kumbukumbu za mahesabu pamoja na kuwajengea uwezo watumishi wa Kitengo cha Uhasibu kupitia Mafunzo mbalimbali. Ushindi huu pia unaonesha weledi wa watumishi wa kitengo hicho kinachoongozwa na CPA Stephen James Dalasia.

# Uteketezaji wa dawa za kulevya

*Juni 2021 hadi Februari 2022 dawa za kulevya zimeteketezwa katika maeneo mbalimbali nchini*



*Kamishna Jenerali wa DCEA, Gerald Musabila Kusaya na wadau wengine wanaotambulika kisheria wakiwa katika zoezi la uteketezaji wa dawa za kulevya lililofanyika kiwanda cha saruji cha Dangote Februari 22, 2022 .* ***Picha zaidi ukurasa wa 16.***

**Na DANIEL Kasokola**

UTEKETEZAJI wa dawa za kulevya hufanyika kwa mujibu wa Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Namba 5 ya mwaka 2015 pamoja na Kanuni zake. Sheria hii inaelekeza kwamba, uteketezaji wa dawa za kulevya unaweza kufanywa baada ya shauri kumalizika Mahakamani na kwa dawa za kulevya zenye tabia ya kubadilika au kuharibika zinaweza kuteketezwa kabla au wakati shauri husika linaendelea Mahakamani.

Uteketezaji wa dawa za kulevya hufanyika kwa namna ambayo hulinda afya na kuzingatia kanuni za utunzaji wa mazingira. Zoezi hilo, hushuhudiwa na wadau mbalimbali walioainishwa kisheria ambao ni Hakimu au Jaji, wawakilishi wa Kamishna Jenerali, Inspekta Jenerali wa Polisi, Mkurugenzi wa Mashtaka, Mkemia Mkuu wa Serikali, Idara ya Usalama wa Taifa, Baraza la Taifa la Mazingira na mtu yoyote atakayeteuliwa na Kamishna Jenerali.

Kuanzia mwezi Juni 2021 hadi Februari 2022 dawa za kulevya zilizoteketezwa Nchini ni bangi, mirungi, heroin, cocaine pamoja na methamphetamine.

Tarehe 22 mwezi Februari mwaka 2022, jumla ya kilo 250.7 za dawa za kulevya ambazo kati ya hizo kilo 51.7 ni heroin na kilo 199 ni mchanganyiko wa heroin na cocaine ziliteketezwa katika kiwanda cha saruji cha Dangote mkoani Mtwara. Uteketezaji huu ulifuatia hukumu ya kesi Namba 25 ya mwaka 2019 iliyowahusisha washtakiwa Mohamed Nyamvi na Ahmad Said Mohamed pamoja na kesi Namba 2 ya Mwaka 2018 iliyowahusisha washtakiwa Sano Sidiki na Tukure Ally ambapo katika Kesi hizo washtakiwa walihukumiwa kutumikia kifungo cha miaka 20 gerezani kila mmoja.

Uteketezaji mwingine ulifanyika tarehe 15 mwezi Juni mwaka 2021 mkoani Mtwara, uliohusisha kilo 355 za dawa za kulevya aina ya Methamphetamine zikiwa ni kati ya dawa zilizokamatwa mkoani Lindi zikiwahusisha watuhumiwa saba ambao ni raia wa Iran.

Tarehe 10 mwezi Desemba mwaka 2021 jumla ya hekari 10 za mashamba ya dawa za kulevya aina ya mirungi ziliharibiwa katika kitongoji cha Kindi, wilaya ya Same mkoani Kilimanjaro.

> **10**
>
> *Jumla ya hekari 10 za bangi ziliteketezwa mnamo tarehe 20 mwezi Julai mwaka 2021, katika kijiji cha Tawi, Wilaya ya Rufiji Mkoani Pwani*

Aidha, tarehe 20 mwezi Julai mwaka 2021, katika kijiji cha Tawi, Wilaya ya Rufiji Mkoani Pwani, jumla ya hekari 10 za bangi ziliteketezwa. Hekari hizo ziliwahusisha watuhumiwa Mshamu Omary Tindwa, Ali Saidi Momboka na Amada Hamadi Tindwa.

Uteketezaji uliofanyika katika kipindi hicho ni zoezi endelevu ambalo limekuwa likifanyika pale inapohitajika. Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya iko mstari wa mbele kutoa taarifa kwa umma juu ya uteketezaji wa dawa za kulevya ili kuondoa dhana potovu iliyojengeka kwa baadhi ya watu wanaodai kuwa, dawa za kulevya zinapokamatwa hurejeshwa na kuuzwa tena mtaani.

# *Matukio katika zoezi la uteketezaji wa kilo 250.7 za dawa za kulevya aina ya heroin na cocaine katika kiwanda cha saruji cha Dangote mkoani Mtwara mnamo tarehe 22 Februari, 2022.*











*Kinu kinachotumika kuteketeza dawa za kulevya.*
***(Picha zote na Daniel Kasokola)***



©Musa NGORONGO JR.
SHULENI NA VYUONI WANAFUNZI PIA HUATHIRIKA KWA MATUMIZI YA DAWA ZA KULEVYA, WAZAZI NA WALIMU TUFUATILIE NYENDO ZAO.
PAMOJA TUCHUKUE HATUA!


MIMI NILIKUWA MRAIBU WA DAWA ZA KULEVYA PENGINE KULIKO HATA NYINYI, LAKINI NIMEWEZA KUACHA NA SASA NATIMIZA MALENGO YANGU!
KUMBE INAWEZEKANA!
KAMA NI HIVYO NAMI NACHUKUA HATUA LEO HII!


BABU, TUFANYE NINI ILI TUSIWEZE KUINGIA KATIKA UTUMIAJI DAWA ZA KULEVYA
WASIKILIZENI WALIMU NA WAZAZI WENU, PIA JIEPUSHENI NA MAKUNDI YASIYOFAA
©Musa NGORONGO JR.


UMEHUKUMIWA MIAKA 30 JELA KWA KOSA LA KUJIHUSISHA NA KILIMO CHA BANGI!
UWIII! NAJUTA! BORA NINGEENDELEA NA KILIMO CHA MAHINDI AMBACHO KIMENIWEZESHA KUSOMESHA WATOTO!
©Musa NGORONGO JR.

## Katuni


BINGWA WA RAP 10,000/-TU
NGOJA NIPATE STIMU KABLA SIJAFAFANYA SHOO!
YEP, SASA BANGI IMEKOLEA. NIKAFANYE SHOO YA KUFA MTU!
ALIPOINGIA...
SEMA YO! YO! YO! YO!
YO! YO! YO!
YOOO!
SEMA OYOOOOOOOO!
DAH! NUSU SAA SASA SIKUMBUKI WIMBO HATA MMOJA! HII BANGI MBONA HIVI!
USITUYEYUSHE! MUDA WOTE HUO HUIMBI TU!?
RUDISHA PESA ZETU! UNALETA BANGI HAPA!
hjabeid@gmail.com

MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA

DCEA

**DIRA YETU:** Kujenga jamii ya Tanzania isiyotumia dawa za kulevya au kushiriki katika biashara ya dawa hizo.

**DHIMA YETU:** Kujenga mfumo bora wa kudhibiti na kupambana na matumizi na biashara ya dawa za kulevya na kuendeleza ushirikiano katika hatua mbalimbali za udhibiti wa dawa za kulevya na kujenga uwezo wa Taasisi na Asasi zisizo za kiserikali katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya.